# Kazi nchini Marekani

**Kazi nchini Marekani ni muhimu sana. Kupata, kupewa, na kudumisha kazi ni ya muhimu kwa maisha yako ya kesho na kuishi nzuri kwa familia yako. Ni njia ya haraka zaidi ya kufikia autosuffisance na ni muhimu kwa mafanikio. Lazima uwe tayari kutafuta kazi kikamilifu utakapowasili Marekani.**




## Kutafuta kazi

Watu wazima wote, wanaume na wanawake, wenye umri wa miaka 18 hadi 64 na wanaoweza kufanya kazi wanapaswa kutafuta kazi kwa bidii. Kwa sababu usaidizi wa serikali una muda na kiasi kidogo, ni muhimu utafute kazi pindi tu ufikapo Marekani.




Kazi haiko garantie na gavmenti. Kupata kazi kunaweza kuchukua wiki au hata miezi, na unaweza kuwa na mahojiano mengi ya kazi. Unapashwa kufanya kazi na mtaalamu wako wa kazi ili kupata kazi na kujifunza ma shauri ya kawaida ya embauche.

Unapashwa kuchukua kazi ya kwanza ambayo utapata, hata kama hailipi vizuri sana au haipo katika eneo lako, ili uweze kujenga historia ya kitaaluma na kuanza kusaidia familia yako. Ikiwa una kataa kukubali kazi iliyotolewa kwako, una hatari ya kupoteza usaidizi wa serikali. Mara nyingi kuna watu wengi wanaotuma maombi ya kazi hiyo hiyo moja, kwa hivyo ni muhimu kuwa tayari kukubali nafasi ya kuingia katika uwanja mpya. Ili kupata expérience professionnelle, unapashwa kukaa katika kazi hiyo hiyo moja muda zaidi ya miezi sita .

# Utamaduni wa kazi nchini Marekani

Marekani inajulikana kama nchi ya fursa kwa wale wanaofanya kazi kwa bidii. Ili kupata kazi bora na yenye malipo makubwa, utahitaji kuzungumza, kusoma, na kuandika Kiingereza na labda kujifunza ujuzi mpya. Ikiwa ulikuwa ukifanya kazi katika taaluma ya upekee katika nchi yako, huenda ukahitaji kufata mafundisho na kupata cheti kabla ya kufanya kazi katika taaluma hiyo nchini Marekani.

Wanaume na wanawake wanafanya kazi nchini Marekani. Wanawake ni nusu ya wafanyakazi, hufanya kazi sawa na wanaume katika ngazi zote, na mara nyingi wanawake husimamia wafanyakazi wa kiume.





Nchini Marekani, watoto walio na umri wa miaka 14 na zaidi wanaweza kufanya kazi kwa muda mfupi, lakini wanaweza kuwa na kikomo cha saa wanazoweza kufanya kazi na aina za kazi wanazoweza kufanya. Katika Marekani, vijana wengi hufanya kazi kwa muda baada ya shule, mwisho-juma, na wakati wa vacances. Marekani ina sheria iliyoundwa kulinda wafanyakazi vijana.

# Haki na responsabilité kwa mambo inayo husu emploi

Nchini Marekani, wafanyakazi wana haki na responsabilité mahali pa kazi. Una haki ya kulipwa kwa kazi yako, na sheria ya kazi hulinda wafanyikazi kutokana na hali zisizo salama za kufanya kazi.

Employeur wako hawezi kukubagua kwa kukunyima kazi au kukataa kupandishwa cheo kwa sababu ya umri wako, ulemavu, hali ya ndoa, kabila au taifa, rangi, dini, au jinsia. Alakini, kazi zingine, kama vile kazi za serikali ku administresheni, zina wezekana tu kwa raia wa Amerika.

Wafanyakazi wana haki ya kufanya kazi katika mazingira yasiyo na ubaguzi na

- unyanyasaji, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kijinsia (tabia isiyotakikana ya asili ya kijinsia inayomfanya mtu akose raha au kutokuwa salama)
- unyanyasaji wa rangi au kidini
- uonevu au intimidation
- kulipiza kisasi kwa ajili ya mtu kuripoti matatizo au kudai haki.

Kama mfanyakazi anayelipwa nchini Marekani, ni responsabilité yako kulipa impôt sur le revenu kila mwaka ili kusaidia mpango zinazotoa huduma kwa watu wote wanaoishi Marekani (kwa mfano, elimu, SNAP, Medicaid, barabara za umma, na vivi hivi). Ni responsabilité yako kulipa impôt ku gouvernement federal na ya jimbo unakoishi. Unaweza kupata mashirika ya ndani yasiyo ya kiserkali ambayo yame izinishwa na Huduma ya Ndani ya Mapato kama tovuti ya usaidizi wa kodi na ni yanaye weza kukusaidia kukamilisha marejesho yako ya kodi kila mwaka.

## MASWALI YANAYO ULIZWA MARA KWA MARA

**Je, nitapokea usaidizi wa kutafuta kazi?**
Mashirika yanaweza kusaidia kutoa huduma ya kazi mahali ambapo umepewa makazi mapya, lakini utakuwa na jukumu kuu katika kutafuta na kudumisha kazi.

**Nitakuwa na kazi ya aina gani?**
Kazi yako ya kwanza huenda isiwe katika taaluma sawa na ile uliyofanya katika nchi yako. Inaweza kuwa ya kiwango cha kuingia, isiyo ya kitaalamu, au hata ya muda. Kwa kuzingatia gharama kubwa ya kuishi Marekani, ni jambo la kawaida, na mara nyingi ni la lazima, kwa wanaume na wanawake kufanya kazi nje ya nyumba.

**Je, namna gani kwenda kazini?**
Public transportation is available in most U.S. cities. You may need to rely on public transportation to access your first job.

## Kuhusu Settle In

Settle In ndicho chanzo chako unachokiamini cha taarifa za kuaminika, sikivu, na muhimu kuhusu Marekani. Inapatikana katika lugha nyingi, mifumo ya kidijitali ya Settle In hutoa nyenzo muhimu, mwongozo, na usaidizi wa lugha nyingi ili kuwasaidia wapya kuendesha maisha nchini Marekani.

## Kuhusu Switchboard

Switchboard ni kitovu cha rasilimali cha watoa huduma kwa wakimbizi nchini Marekani na inatoa zana, fursa za kujifunza na usaidizi wa kiufundi kuhusu mada zinazohusiana na uhamishaji.

Inafadhiliwa na ORR, Switchboard inatekelezwa na IRC.

IRC ilipokea ufadhili wa kiushindani kupitia Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu ya États-Unis, Utawala wa Watoto na Familia, (subvention n° 90RB0053).

Mradi huo unafadhiliwa kwa 100% na fedha za shirikisho. Yaliyomo katika waraka huu ni jukumu la waandishi pekee na si lazima yawakilishe maoni rasmi ya Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu ya Marekani, Utawala wa Watoto na Familia.

switchboard
connecting resettlement experts

SettleIn